

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 7 Juni, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae,
Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Kama kawaida yetu tunaanza na maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu sasa aulize swali lake. Kwa niaba Mheshimiwa Lubeleje.

Na. 350

**Maombi ya Kupata Wilaya/Halmashauri – Jimbo la
Ulyankulu**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y MHE. JOHN P.
KADUTU)** aliuliza:-

Kumekuwa na maombi ya kupata Wilaya na Halmashauri ya Ulyankulu kwa muda mrefu sasa. Pia

zimetolewa ahadi za kuunda Wilaya na Halmashauri tangu mwaka 2010.

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi Wilaya na Halmashauri kwani vigezo vya kuwa Wilaya/Halmashauri ni kama vile vya Jimbo ambavyo tayari vimetimia?

(b) Je, ni kikwazo gani kimesababisha kutopata Wilaya/Halmashauri mpaka sasa?

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya kuanzisha Wilaya ya Ulyankulu ya mwaka 2010 hayakufanikiwa kutokana na kutokidhi vigezo vikiwemo idadi ya watu pamoja na sehemu kubwa ya eneo hilo kuwa ni hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maombi ya mwaka 2010 hayakukidhi vigezo na kwa sasa kama Halmashauri inaona eneo hilo limekidhi vigezo hivyo, tunashauri Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kuanzisha mchakato wa kujadili mapendekezo hayo upya na kuyapitisha katika Baraza la Madiwani na Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa na hatimaye kuwasilisha Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ili yaweze kufanyiwa kazi. Serikali haitasita kuridhia pendekezo hilo endapo litakuwa limekidhi vigezo na taratibu zilizokuwa zimewekwa kwa mujibu wa Sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Kadutu la Ulyankulu linafanana kabisa na Tarafa ya Mima ambayo imeshatangazwa kwamba imeanzishwa kuwa Tarafa ya Mima, lakini mpaka sasa hakuna majengo, hakuna watumishi. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini mtajenga majengo, mtaleta watumishi ili kweli ile Tarafa ya Mima ianze kufanya kazi mara moja maana sasa inatamkwa tu Tarafa ya Mima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Kata za Matomondo pamoja na Mlembule ni kata kubwa sana na zina vigezo vyote kuwa tarafa, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, unasemaje kuhusu hili? Ni lini mtaanzisha Tarafa hizi Kata mbili, Mlembule na Matomonda?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la *Senior MP* Mheshimiwa Lubeleje ambaye mimi namuita *grader* la zamani makali yale yale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika Tarafa ya Mima ambayo kwa mujibu wa utaratibu Mheshimiwa amesema kwamba imeshaanzishwa lakini majengo ni bado. Basi mimi naomba nielekeze katika Halmashauri husika kwa sababu nadhani wakati tunafanya mchakato wa kuanzisha tarafa hizi ni lazima tutakuwa tumejipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nafahamu kwamba unafanya juhudi kubwa, lakini niwasihi wenzetu kule, kwa sasa hivi iangalie namna ya kufanya katika mipango ile ikiwezekana ya Kihalmashauri na Kiwilaya. Katika maana hiyo tuanze michakato ya kuanzisha majengo kwa kuangalia suala zima la ki-bajeti. Jambo hili linaanzia kule kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wakati wa mchakato wa bajeti na sisi tutaunga mkono suala la watumishi; ambayo ndiyo mamlaka yetu kupeleka watumishi

kama Serikali. Nikuhakikishie Mheshimiwa Lubeleje kwamba jambo hili tutalifanya kwa kadiri taratibu za Serikali zinavyokwenda sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzishwa tarafa mpya katika Kata ya Matomondo na. Najua kwamba michakato hii iko vile vile kwa mujibu wa Sheria za uanzishwaji wake. Kwa sababu hiyo basi nishauri Baraza la Madiwani kwamba jambo hili likionekana linakidhi sasa katika Halmashauri yetu ya Mpwapwa basi liweze kufanyika katika ile michakato ya kimsingi ambayo inaanzia katika vijiji inakuja katika vikao vya *Ward C*, na Halmashauri ya Wilaya *then DCC* ya wilaya na Mkoa, baadaye inakuja Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa maamuzi zaidi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Lubeleje naomba nikuhakikishie kwamba mkianza mchakato huo Ofisi ya Rais TAMISEMI itasikiliza kilio chenu na kuweza kukifanyia kazi kwa kadri inavyoona inafaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanne.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mchakato wa uanzishwaji wilaya ni wa muda mrefu na hili swali sasa ni la mara nyingi tunauliza; kwa kuwa Ulyankulu ilikuwa na makazi ya wakimbizi, na ambao wapo mpaka sasa, na kwamba vile vile wapo wakimbizi ambao wamepewa uraia na kusababisha kuongezeka kwa idadi ya watu na kuwa na watu wengi.

Je, Serikali haioni hilo? je, ni lini sasa inaweza ikaamua kwa maksudi kuhakikisha kwamba wilaya ile sasa inakuwepo baada ya kukamilisha vigezo vyote tulivyovileta. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale awali, mapendekezo ya kwanza yalivyokuja ikaonekana kuna mapungufu ya idadi ya watu, hii ndiyo iliyokuwa miongoni mwa vigezo ambavyo vilifanya isi-*qualify* kipindi kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amekiri hapa kwamba kuna baadhi ya makazi ya wakimbizi, nadhani takriban kata tatu, zimesababisha kuwepo kwa sasa idadi kubwa sana ya watu katika maeneo hayo ambayo sasa wamesajiliwa kuwa kama raia wa Tanzania. Hata hivyo utaratibu ni ule ule kwa sababu lile jambo la mwanzo lilidondoka haliku--*qualify*. Kwamba kama tunaona idadi sasa hivi inatoshwa twende na michakato ile ile kama nilivyosema awali, kwamba ipitishwe katika vikao vya kisheria ambavyo katika *Ward C, DCC* pamoja na *RCC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikifika kwetu sisi, tutawatuma wataalam kuja kufanya *verification*, iki-*qualify* biashara imekwisha. Kwa hiyo mama Mwanne Mchemba naomba nikutoe shaka katika hilo, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) itasikiliza jambo hili na kwa kupitia *document* zote zilizotumwa kutoka kwenu tutalifanya kazi jambo hili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Massare atafuatiwa na Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyopo huko Wilaya ya Ulyankulu yanafanana kabisa na matatizo yaliyoko katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi. Jimbo la Manyoni Magharibi ni Tarafa ya Itigi ambayo ina upana mkubwa, eneo moja mpaka eneo lingine ni kilometa 219, ni jimbo kubwa kuliko majimbo mengi. Tumeshapeleka na kupitia taratibu zote hadi *RCC* kuiombea Itigi kuwa Wilaya lakini hadi leo

Serikali imekuwa kimya. Je, Serikali inasema nini kuhusu jambo hili la Wilaya ya Itigi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Kwanza awali hata hili eneo la Itigi tulikuwa hatujapata Halmashauri kamili na ndiyo maana mchakato wa kwanza ulikuwa ni kupata Halmashauri. Suala hili najua Mheshimiwa Massare umelizungumza mara nyingi tangu uchaguliwe kuwa Mbunge. Naomba nikuhakikishie kwamba tutafanya *verification* katika ofisi yetu kuona hizi *document* ziko katika *process* gani. Kama hali haijawa sawa sawa tutatoa maelekezo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwamba ikamilishe zile taratibu nyingine zote ambazo zitakuwa zimefungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakumbuka kwamba Mheshimiwa Mbunge tulifika pale Itigi na kweli ukiangalia jiografia hata aliyekuwa Mkuu wa Wilaya wa kule ambaye sasa hivi ndiye Mkurugenzi wetu Mkuu wa *TIC* alikuwa anapata changamoto kubwa sana kui-*manage* ile Wilaya ya Manyoni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Massare naomba nikuhakikishie kwamba mambo haya yote yakikamilika, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) itakapojiridhisha, haitasita kufanya maamuzi kwa maslahi mapana ya eneo lako husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nia kubwa ya kugawa maeneo ni kusogeza huduma kwa wananchi na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri baada ya sisi wananchi wa Kilolo kupige kelele kutokana na ukubwa wa Wilaya yetu, uliridhia na kutupa Halmashauri ya Mji Mdogo sasa ni muda mrefu na ulifika na kuona kwamba sasa tunastahili kupata Halmashauri kamili. Je, ni lini sasa Mheshimiwa? Hebu tupe jibu ili wananchi wakusikie.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Mwaka jana tulikwenda na Mbunge tukafika mpaka jimbo lake, tukatembea. Kijiografia jimbo lile ni kubwa sana, linapakana na ndugu yangu Profesa Jay, linapakana na Waziri wangu Simbachawene huku Kibwakwe, ni jimbo ambalo liko tata kweli kweli. Hata hivyo tulivyofika pale Ilula tumekutana na wananchi wa Ilula ambao mapendekezo yao yametufikia, na bahati nzuri baada ya ile ziara nikatuma timu kwenda kufanya *verification*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *verification* imeshafanyika na hivi sasa tuko katika mchakato wa kufanya maamuzi ambapo kwa jambo hili mwenye kufanya maamuzi ni Mheshimiwa Rais mwenyewe mwenye dhamana katika eneo hilo, atakaporidhia basi Mheshimiwa Mwamoto naomba usiwe na hofu, ni kweli Serikali imefanya *process* zote na sasa tuko katika *final stage* katika kufanya maamuzi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Namalizia kwa Mheshimiwa Amina.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Arumeru ina Halmashauri mbili kwa maana kwamba Halmashauri ya Meru na *Arusha DC*. Wilaya hii eneo lake ni kubwa kiasi kwamba hata wakati mwingine huduma kuzifikia jamii inakuwa ni vigumu. Je, ni lini sasa Serikali (kwa sababu tayari ilikwishaanza mchakato siku za nyuma) itaendelea na mchakato huo kuhakikisha kwamba inagawanya wilaya hii inakuwa wilaya mbili ili huduma za kijamii ziweze kuwafikia wananchi kwa haraka? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la dada yangu Amina Mollel Mbunge ambaye anawakilisha hasa kundi la walemavu kwa umakini zaidi humu Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wilaya ya Meru ni kubwa sana, ina *Arusha DC* na Meru. Ukiangalia, bahati mbaya Halmashauri ile iko kama mbalamwezi fulani hivi, kwamba Jiji la Arusha liko katikati halafu ile wilaya imezunguka hivi. Kwa hiyo hata *management* yake inakuwa ni ngumu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kama nilivyosema katika maeneo mbalimbali, kwanza naamini michakato mbalimbali imeanza huko lakini wakati mwingine inawezekana taarifa zikawa zimekuja lakini vigezo havikukidhi. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Amina Mollel kwamba tutakapopata taarifa za vikao vya *RCC* kutoka Mkoa wa Arusha na Mkuu wetu wa Arusha akishajipima kule akiona kwamba jambo hilo limeridhia, na likishafika kwetu na sisi tatalifanyia kazi kufanya taratibu zote za kisheria zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikionekana kwamba inafaa sasa kuigawanya zile wilaya mbili, Serikali itaona jinsi gani ya kufanya katika hilo. Kwa hiyo naomba nikuhakikishie, ni kwamba utaratibu ni ule ule wa kisheria tu, kama unavyosema ugawanyaji wote wa maeneo unasemaje. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana wa eneo hilo akiridhia, basi mchakato utakamilika hatimaye mtapata wilaya mpya.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 351

**Kuanzisha Kidato cha Tano na Sita Sekondari ya
Yitwimila "A"**

MHE. GIMBI D. MASABA aliuliza:-

Kampuni ya *Group Sogesca Lanari Estero (GSLE)* iliyokuwa inajenga barabara ya Nyanguge – Musoma kati ya mwaka 1979 – 1990 iliacha majengo katika Kijiji cha

Yimtwila "A" ambapo Serikali kwa kushirikiana na wananchi wakaanzisha shule ya sekondari ya kutwa.

Je, ni kwa nini Serikali isitumie fursa ya uwepo wa majengo haya kupandisha hadhi shule hiyo kuwa ya kidato cha tano na sita kwa kuwa nyumba za walimu na mabweni yanaweza kupatikana?

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo yaliyokuwa kambi ya Kampuni ya *Group Sogesca Lanari Estero* iliyokuwa inajenga barabara ya Nyanguge kwenda Musoma kati ya mwaka 1979 hadi 1990 kwa sasa yanatumika kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Sogesca ambayo ni ya kutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha uwepo wa shule ya kidato cha tano na sita Wilayani Busega, Serikali imeweka kipaumbele cha kuanzisha shule ya sekondari Mkula kuwa ya kidato cha tano na sita katika mwaka wa fedha 2016/2017. Tayari Serikali imepeleka shilingi milioni 259 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wanafunzi, vyumba vya madarasa vinne, matundu ya vyoo kumi na ukarabati wa maabara. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha shule za sekondari za kidato cha tano na sita zinaanzishwa katika kila tarafa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gimbi kama una swali lolote.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri wazi kwamba Serikali ina mpango wa kuanzisha shule ya kidato cha tano na cha sita katika maeneo ya Mkula tofauti na maeneo yanayotumika kwenye majengo yaliyoachwa na Kampuni ya *Group Sogesca*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; itambulike kuwa shule hii ambayo ameizungumzia kwamba ni ya kutwa iko kwenye mgogoro baina ya wananchi pamoja na Kampuni ya SK iliyoko mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu Mheshimiwa Waziri Mkuu anaujua. Alipokuja kwenye ziara tarehe 2 mwezi wa tatu mwaka wa jana aliukuta mgogoro huu wa wananchi, kwamba shule hii iko kwenye majengo ambayo yana mgogoro. Nataka kusikia kauli ya Serikali, Waziri Mkuu aliagiza kuwa majengo yale yarudi kwenye mikono ya wananchi ili shule ile iweze kuendelea vizuri. Sasa nataka kuuliza, nini kauli ya Serikali kuhusu shuke iliyoko kwenye majengo yenye mgogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa kipaumbele cha Serikali ni masomo ya sanyansi. Mkoa wa Simiyu walimu wa masomo ya sayansi ni changamoto kubwa sana hususan shule iliyoko Wilayani Itirima, shule ya Mwarushu ina mwalimu mmoja tu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusikia sauti ya Serikali ni nini mkakati wa Serikali kupeleka walimu wa sayansi katika maeneo hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Dada yangu Gimbi Dotto, kumbe alikuwa anataka aniingize katika choo kisichokuwa na jinsia maalum, kwamba shule kumbe ina mgogoro halafu tuanzishe kidato cha tano na cha sita. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna mgogoro lakini nadhani Naibu Waziri wa Ardhi atazungumzia hasa katika suala hili la mgogoro jinsi gani Serikali imejipanga mara baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa maagizo; Serikali inayafanyia kazi hayo yote kwa pamoja na nikuhakikishie Mheshimiwa Gimbi kwa sababu najua wewe ni mpiganaji mpaka umeniletea walimu ambao walikuwa na matatizo katika eneo lako kule. Siku zote unaniletea taarifa ofisini kwangu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba tutashughulikia matatizo katika Mkoa huu wa Simiyu kwa kadri iwezekanavyo ili mambo ya elimu yaende vizuri. Kuhusu shule ambayo haina walimu wa sayansi, naomba tuseme kwamba katikati tulipeleka walimu wa sayansi lakini si kwamba tumeziba *gap* zote za walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunaendelea kupeleka walimu wa sayansi. Tutaichukulia hii shule ambayo unaisemea kuwa ni kipaumbele, tutafanya kila liwezekanalo ili kuhakikisha kwamba tunapeleka walimu wa sayansi wa kutosha. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba watoto wanapata elimu vizuri. Kwa hiyo naomba uendelee na hizo juhudi zako nzuri za kuwawakilisha vizuri wananchi wako wa kule.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swali dogo la nyongeza ambalo limeulizwa. Ninamshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye amejibu swali lake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mbunge pengine wakati mwingine ni muhimu pale ambapo Serikali inachukua hatua tuwe tunaweza kuweka kumbukumbu zetu vizuri. Mgogoro huu anaouzungumzia tayari Serikali ilishaumaliza, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Lukuvi alishakwenda kule

na yule Bwana alinyang'anywa *title* yake na Mheshimiwa Rais alishaifuta, kwa hiyo hakuna mgogoro pale na *SK Investment* si mmiliki tena wa eneo lile kwa sababu Serikali imeshafuta umiliki wake na ilitangazwa kwenye vyombo vya habari, naomba tuwe tunafuatilia vizuri ili tusiwe tunachanganya haya mambo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Chegeni wa mwisho.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Shule hii iliyotajwa na Mheshimiwa Gimbi na ninapenda nimshukuru kwa swali lake, lengo lake ni kwamba kuipandisha kuwa *high school*, lakini kwa mpangilio wa Wilaya ya Busega tumeipanga kuwa ni Chuo cha *VETA*. Je, ni lini Serikali kupitia Wizara ya Elimu itatusaidia kuwa na shule ya *VETA* katika majengo haya Sogesca?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ipo tayari kwa kila fursa inayojitokeza, kwa hiyo tutaenda kuangalia kuona kama inafaa, basi tutafanya hivyo.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 352

Hitaji la Mikopo kwa Wachimbaji Wadogo – Ruangwa

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH aliuliza:-

Mji wa Ruangwa Mkoani Lindi una madini mengi lakini wachimbaji walio wengi wa madini hayo ni wachimbaji

wadogo wadogo ambao hawana zana za kisasa za kuchimba madini.

Je, Serikali haioni haja ya kuwasaidia kwa kuwapa mikopo ili waweze kununua zana za kisasa za uchimbaji?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalaum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini imeweka vipaumbele vya kusaidia wachimbaji wadogo ili kufanya shughuli zao za uchimbaji huo kuwa wa manufaa kwao pamoja na kuongeza pato la Taifa. Vipaumbele hivyo ni pamoja na kuboresha sekta ya uchimbaji madini mdogo kwa kutoa ruzuku kwa wachimbaji hao wadogo ili waweze kuboresha shughuli zao kuwa za kisasa na kuboresha uchenjuaji na shughuli nyingine za uchimbaji. Lakini vipaumbele vingine ni kuwapa ushauri wa kitaalamu, taarifa za upatikanaji wa vifaa vya uchimbaji, mafunzo kwa vitendo pamoja na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2010 na 2013 Serikali ilitoa mikopo ya jumla ya shilingi milioni 910.195 kwa kampuni nane za wachimbaji wadogo. Aidha, kati ya mwaka 2013 na 2015 Serikali ilitoa ruzuku ya shilingi bilioni 678.178 kwa wachimbaji 115 kwa ajili ya uchimbaji wao nchi nzima pamoja na Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianza kutoa ruzuku badala ya mkopo kwa wachimbaji wadogo kutokana na wachimbaji wadogo kushindwa masharti ya mikopo na hivyo kushindwa kurejesha na badala yake sasa wanapewa ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele muhimu vinavyozingatiwa katika kutoa ruzuku hiyo ni pamoja na kumiliki leseni hai na halali ya shughuli za uchimbaji, kuwa

na utambulisho wa kodi na mlipa kodi (*TIN*) na rekodi nzuri ya kulipa mrabaha na mapato mengine ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Jiolojia Tanzania wataendelea kufanya utafiti wa maeneo yote nchini ili wachimbaji wadogo nao sasa waweze kunufaika na rasilimali hii ya Taifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamida swali la nyongeza.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu haya ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini na Nishati, majibu ya jumla ambayo yanaelekeza katika maeneo yote ya uchimbaji wa madini, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika Mkoa wetu wa Lindi tunayo madini mbalimbali lakini katika eneo hili la Wilaya ya Ruangwa tuna madini ya *green gannet*, *green tomalin*, dhahabu, safaya na *graphite* pamoja na madini mengine, lakini maeneo haya wachimbaji waliopo ni wachimbaji wadogo wadogo ambao wanatumia zana ambazo si bora, zana hafifu.

Ningependa kujua tunayo Sera na Sheria Mpya ya Madini ya kuwatengea maeneo wachimbaji hao wadogo wadogo, sera hii imewanufaisha vipi na Sheria mpya ya Madini wachimbaji wadogo wadogo wa maeneo hayo ya Wilaya ya Ruangwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza ningependa kumuomba Mheshimiwa Waziri, yupo tayari sasa kuja katika Mkoa wetu wa Lindi maeneo ya Ruangwa kuja kuona maeneo ya machimbo haya ya madini na kuona changamaoto mbalimbali zinazowakumba wachimbaji hao wadogo wadogo na kuona namna gani Wizara yake inaweza kuwasaidia? Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote sio tu nipo tayari kwenda Lindi isipokuwa nipo tayari kufuatana na Mheshimiwa Hamida twende pamoja mpaka Lindi. Kwa hiyo kwa ruhusa ya Kiti chako nipo tayari na ukitupa ruhusa hata kabla ya Bunge kumalizika nipo tayari Mheshimiwa Mbunge kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Hamida Abdallah anavyoshughulikia masuala haya, tangu ameingia katika Bunge hili tumeshashirikiana naye sana na katika juhudi zake amefanikisha kutenga maeneo mawili muhimu sana katika Mkoa wa Lindi, eneo mojawapo ni Kitowelo pamoja na eneo la Maguja Nachingwea, kwa hiyo, Mheshimiwa hongera sana kwa kazi zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mkoa wa Lindi una madini mengi sana, baadhi ya madini yanayopatikana katika Mkoa wa Lindi kama alivyoyataja Mheshimiwa Mbunge ni pamoja *green tomaline*, *safaya* pamoja na madini *load garden*, lakini kuna dhahabu, kuna chumvi kuna madini mengi yanayoitwa *ruby* ambayo ni madini ya mfano sana katika nchi yetu. Kwa mkoa wa Lindi una utajiri wa madini mengi tu pamoja na chumvi. Nichukue nafasi hii kuwahamsisha sana Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Lindi na maeneo mengine ili kuhamasishe wachimbaji wadogo wakachimbe madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera na sheria kweli kabisa zinataja kuwatengea maeneo wananchi nchi nzima. Katika Mkoa wa Lindi tumeshatenga maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetenga eneo la hekta 300 Kilwa Masoko kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya chumvi, tumetenga maeneo ya hekta 525 eneo la Kitowelo katika Wilaya ya Liwale na eneo la kilometa 7.2 katika eneo la Maguja Wilaya ya Nachingwea na tunakwenda sasa kutenga eneo lingine la hekta 825 katika eneo linaitwa Hoteli Tatu. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge tunaendelea kutenga maeneo kama na sera ya madini inavyoelekeza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecil Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kwa kuuliza swali la nyongeza, linalohusiana na masuala ya madini kama ambavyo Mheshimiwa Hamida ameuliza hapo mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo Ruangwa linafanana kabisa na tatizo lililopo Jimbo la Ndanda katika kijiji cha Chiwata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Chiwata sasa hivi kuna uwekezaji unaendelea kwa ajili ya madini ya *graphite*, lakini uwekezaji huu umekuwa ukufanyika kwa siri kubwa sana kiasi kwamba wananchi wa Chiwata hawafahamu nini kinaendelea na hawako tayari kuendelea kukaa kimya, wamenituma nimuulize Waziri.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuleta mkataba ambao utatumika kwa ajili ya uchimbaji wa madini katika kijiji cha Chiwata ili kuondoa sintofahamu ambayo inaweza ikajitokeza miaka ya baadaye ya kuhitaji kufanya *review* na ku-*cancel* mikataba ile? Ninaomba *commitment* ya Serikali ni lini iko tayari kuleta mkataba ule ujadiliwe na Bunge ili ukatumike kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Jimbo la Ndanda? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mwambe nampongeza sana, tumekuwa tukishirikiana naye sana kwenye masuala ya wachimbaji wadogo mbali na masuala yake ya masuala ya nishati kwenye eneo lake. Kuhusiana na eneo analolitaja yuko mwekezaji ambaye sasa anajiandaa na kukamilisha utafiti, atakapokamilisha utafiti ndio aanze shughuli za uchimbaji, kwa hiyo hata hatua ya kuingia mkataba bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nikuombe sana Mheshimiwa tukae, tujue kitu gani kinahitajika na itakapofikia wakati wa kuingia mikataba tukushirikishe, sasa ni lini

mkataba tutaleta nadhani bado sana kuzungumza jambo hilo akamilishe utafiti, akishaanza uchimbaji akaingia mikataba tutajadiliana, kama kutakuwa na haja ya kuuleta basi tutaona ni utaratibu gani utumike ili Mheshimiwa Mbunge kuweza kuuona mkataba huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aysharose.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuniona. Tatizo lililopo Ruangwa halina tofauti na tatizo lililopo Manyoni Magharibi, kwa kuwa sasa kuna Sera ya Madini inayotaka kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo wa madini ruzuku.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa ruzuku kwa wajasiriamali wachimbaji wa *gypsum* wa Wilaya ya Itigi ili kuongeza uzalishaji na hata kuanzisha viwanda? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikupongeze Mheshimiwa Matembe, Mkoa wa Singida na hasa katika maeneo ya Itigi kuna maeneo mengi sana ambayo kuna madini ya dhahabu na katika maeneo hao kwa mwaka jana tumepatia ruzuku wachimbaji wadogo 32, lakini tunaendelea pia kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mbunge kushirikishe tu, tutakapofikia hatua sasa ya kugawa ruzuku nyingine awamu ya tatu ambayo ipo kwenye maandalizi tutakushirikisha na tunatarajia kuanzia mwakani taratibu zikikamilika tutaanza kukamilisha utaratibu mwingine wa kuwapatia ruzuku pamoja na mikopo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka tunamalizia.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la

nyongeza. Kama ambavyo Naibu Waziri ameitambua Kitowelo kwamba atatenga kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Vilevile eneo hilo liko ndani ya kijiji cha Lilombe, lakini tangu uchimbaji huu mdogo umeanza kijiji kile cha Lilombe hakijawahi kunufaika kwa lolote na Halmashauri nzima ya Liwale hajjawahi kunufaika kwa lolote, kwa sababu vibali vya uchimbaji vinatoka Kanda, halafu wale wakitoka kwenye Kanda wanaingia moja kwa moja vijijini wanaanza uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, nini kauli ya Serikali juu ya manufaa wanayoyapata vile vijiji ambavyo tayari machimbo hayo yapo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakiri jambo ambalo anazungumza na tumezungumza naye kama miezi miwili iliyopita, nikaomba sana nimuagize Mheshimiwa Mkurugenzi wake na Watendaji wa Vijiji ili watumie fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wote nchi nzima, wadogo na wakubwa wanatakiwa kutoa ushuru wa Halmashauri husika, wanatakiwa kuchangia maendeleo ya vijiji ambayo shughuli za uchimbaji zinafanyika. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Mbunge ikiwezekana nitakafanya ziara huko tutaita mkutano chini ya Mkurugenzi wako, Watendaji wote wa Serikali ambao shughuli za migodi zinafanyika ili sasa Serikali za Vijiji vianze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ni kwamba kila kijiji ambapo kuna mgodi wa aina yoyote mkubwa na mdogo lazima wachimbaji hao washiriki katika shughuli za maendeleo.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri

wa Nishati na Madini, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa sasa aulize swali lake.

Na. 353

Serikali Kupunguza Matumizi Yasiyo ya Lazima

MHE. JAPHET N. HASUNGA aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya Serikali na Taasisi zake.

Je, Serikali inategemea kuchukua hatua gani ili kutekeleza azma hiyo ya kudhibiti matumizi ya fedha za umma katika taasisi zake?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imechukua hatua kadhaa katika kuboresha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma hususan katika kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Hatua zilizochukuliwa zimegawanyika katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza ni kutungwa kwa sheria mbalimbali na Bunge lako Tukufu na kundi la pili ni miongozo mbalimbali iliyotolewa na Msajili wa Hazina katika utekelezaji wa majukumu yake ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu ni pamoja na Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015, ambayo imebainisha hatua mbalimbali za kibajeti zenye lengo la kuongeza usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma katika mashirika na taasisi za umma. Pamoja na masuala mengine, sheria hiyo

imebainisha utolewaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti (*Plan and Budget Guidelines*) wa Serikali unaojumuisha mashirika na taasisi zote za Serikali ambao unatoa miongozo mbali mbali ya kuzingatwa katika matumizi ya Umma kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia sheria hiyo, Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa mamlaka ya kupitia bajeti za mashirika na taasisi zilizo chini yake kwa kuzingatia miongozo na mipango ya Serikali inayotarakiwa kutekelezwa. Pia Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa jukumu la kupitia na kuridhia kanuni za fedha (*financial regulations*) za mashirika na taasisi zote za umma ili kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingine iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu ni marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 ambayo iliweka ukomo wa taasisi na mashirika ya umma kutumia asilimia 60 tu ya mapato yake kwa matumizi ya kawaida yasiyojumuisha mishahara. Aidha, kati ya asilimia 40 inayobaki, asilimia 70 ya fedha hizo inarejeshwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msajili wa Hazina katika kutekeleza majukumu yake ya kisheria ametoa miongozo mbalimbali yenye lengo la kudhibiti matumizi ya mashirika na taasisi za umma kama ifuatavyo:-

(i) Barua iliyotolewa na Msajili wa Hazina tarehe 10 Novemba, 2015 ya kudhibiti safari zisizo za lazima nje ya nchi kwa watumishi wa mashirika na taasisi za umma ambazo awali zilionekana kutumia sehemu kubwa ya fedha za umma.

(ii) Waraka wa Msajili wa Hazina Namba 12 wa mwaka 2015 kuhusu Posho za Vikao vya Bodi ya Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi za Umma. Waraka huo umefuta posho za Vikao vya Bodi na kuondoa utaratibu wa Bodi kuwa na vikao zaidi ya vinne kwa mwaka mmoja.

(iii) Waraka wa Msajili wa Hazina Namba 1 wa mwaka 2016 kuhusu posho za kujikimu kwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi za Umma. Waraka huo uliweka ukomo wa posho hizo kwa Wajumbe wa Bodi kwa safari za ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kusimamia na kufuatilia miongozo yote inayotolewa na Serikali ili kuhakikisha kuwa lengo la kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima kwenye mashirika na taasisi za umma linafanikiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasunga na baadae Mheshimiwa Ndugulile.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na hatua ambazo zimechukua katika kudhibiti matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya eneo ambalo limekuwa na matatizo makubwa katika taasisi za umma ni eneo linalohusu ununuzi wa vipuri na matengenezo ya magari pamoja na mafuta.

Swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote walioko katika Menejimenti za Mashirika hayo wanakopeshwa magari badala ya kutumia magari ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndiye mwenye wajibu wa kukagua hesabu zote za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma, lakini kwa muda mrefu tumeona kwamba hesabu za taasisi za umma, Mkaguzi Mkuu amekuwa akizipatia sekta binafsi zimekuwa zikikagua kwa niaba yake, lakini sekta hizo binafsi zimekuwa ziki-charge fedha kubwa sana ya ukaguzi.

Je, ili kupunguza matumizi Serikali ina mpango gani

wa kuimarisha ofisi ya CAG ili iweze kufanya kazi hiyo sawa sawa badala ya kutumia sekta binafsi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ununuzi wa vipuri na matengenezo na watumishi kukopeshwa magari, tunapokea wazo lake zuri na tutalifanyia kazi kuona ni jinsi gani utekelezaji wake ili kuona tunapunguza matumizi haya kama alivyosema kwenye magari. Tuisahau pia ni taratibu na kanuni za utumishi ndizo ambazo zinaelekeza haya yote ambayo yanatendwa na Serikali yetu, pale ambapo itaonekana inafaa tofauti na uamuzi uliopo sasa, basi Serikali yetu haitasita kufanya hivyo ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kama ambavyo Serikali imekusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu Serikali yetu inatambua umuhimu wa ofisi hii ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na imekuwa ikiimarisha kila mwaka hatua kwa hatua kuhusu wafanyakazi kupewa ujuzi lakini pia kuhusu na bajeti yake. Sote ni mashahidi tumeona juzi tumepitisha bajeti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na imeongezeka kama Bunge lako Tukufu ambavyo ilipendekeza, ni imani yangu ofisi hii itakagua ofisi zetu na taasisi zote za umma pale ambapo inaonekana inafaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndugulile atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NGUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dhana ya kupunguza matumizi ya fedha na kubana matumizi katika Serikali, Serikali imekuwa inanunua magari kutoka kwa ma-*dealers*, magari haya huwa yanakuja na *warrants* ya kilometa laki moja au

miaka mitatu matengenezo yanakuwa bure, lakini *warrant* hii Serikali imekuwa haitumii na badala yake imepeleka magari kwenye *garage* za watu binafsi na kutumia gharama kubwa sana.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwanza inasimamia hizi *warrant*, ikiwa ni pamoja na kuwa na mpango wa kununua magari kutoka kwa *manufactures*?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wake tutaenda kuufanyia kazi na baadae tutamletea majibu stahiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kujaribu kueleza sheria mbalimbali za kudhibiti fedha za umma, lakini kuna changamoto moja kubwa. Ofisi ya Mkaguzi na Mdhhibiti wa Hesabu za Serikali ndio mtu pekee ambaye amekuwa akisimamia na kudhibiti hili suala la umma na kutuonesha wapi kwenye mapungufu na matumizi sahihi. Lakini Serikali imekuwa haipeleki fedha za kutosha kwa CAG ili aweze kudhibiti hizi fedha.

Je, Serikali haioni kwamba yenyewe ndio yenye jukumu la kuzorotesha Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kushindwa kufanya kazi yake ili tuweze kujua hayo mapungufu, kwa kushindwa kupeleka hizo fedha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu swali la pili la Mheshimiwa Hasunga kwamba Bunge hili hata wiki haijapita tangu tumepitisha Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango,

ndani yake ikiwepo bajeti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na sote tumeona *commitment* ya Serikali yetu katika kuiongezea ofisi hii bajeti ya kutosha. Katika taasisi zote za Serikali ni taasisi hii tu ambayo imepata bajeti yake kwa mwaka huu kwa zaidi ya asilimia mia moja. Hii ni *commitment* ya kutosha kabisa na tunahakikisha kwamba itaendelea kuimarishwa kama nilivyosema. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini.

Na. 354

Usalama wa Wasafiri Kati ya Bandari ya Tanga na Mkokotoni

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu sasa Bandari za Tanga na Mkokotoni zimekuwa zikitumika na kusababisha maafa makubwa kwa watumiaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha usalama wa wasafiri hao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa wakazi wa maeneo ya Tanga, Visiwa vya Unguja na Pemba wanapata huduma bora na salama na hivyo kuwaepusha na usafiri wa vyombo

vya majini visivyokidhi matakwa katika kubeba abiria na mizigo. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na:-

(i)Kuhakikisha kuwa vyombo hivyo ni salama kabla havijaanza kutoa huduma. Kwa sababu hiyo *SUMATRA* hufanya ukaguzi wa lazima (*Statutory Inspection*) wa vyombo kila baada ya mwaka ili kubaini kwamba vyombo hivyo vinaendelea kukidhi ubora na usalama wa kuelea majini. Aidha, *SUMATRA* hufanya kaguzi za kushtukiza ili kuhakikisha kuwa vyombo vya majini vinaendelea kuwa salama wakati wote.

(ii) Kuweka na kutekeleza mikakati ya namna ya kudhibiti uibukaji na matumizi ya bandari bubu katika mwambao wa Pwani kwa kuwa vyombo vingi vinavyoanza safari zake katika bandari zisizo rasmi siyo rahisi kufuata masharti ya ubora na usalama wa kuelea majini. *SUMATRA* inashirikisha uongozi wa Serikali za Vijiji na Kata, vikundi vya kudhibiti uvuvi haramu na usimamizi wa mazingira ya mialo ambao husaidia kusimamia utaratibu wa uondokaji wa vyombo katika mialo ili kuhakikisha vyombo vinavyotumika vinatambulika na kuacha taarifa ya orodha ya abiria na mizigo.

(iii)Kuhimiza sekta binafsi kuwekeza katika utoaji wa huduma za usafiri kwa kutumia meli za kisasa kati ya Tanga, Unguja na Pemba ili wananchi wapate huduma bora na za kutosha kupitia bandari rasmi hivyo kuondoa mazingira yanayolazimisha kutumia bandari bubu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Muhammed swali la nyongeza.

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ambayo hayako makini, majibu ambayo hayaendi sambamba na swali langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mantiki ya swali langu lililenga usalama wa wasafiri pale na mali zao. Kwa kipindi

kirefu sasa wananchi wanaotumia bandari mbili hizi, kila bahari inapopata michafuko kidogo wamekuwa wakifa kwa wingi sana pale.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inathibiti vifo vya watanzania katika bandari mbili hizi ambao mara kwa mara wanapotea wao na mali zao?

Swali langu la pili la nyongeza, inaoneka Serikali haikufanya utafiti wa kutosha. Swali langu halilengi ubora wa bandari, linalenga usalama wa raia wetu pale kati ya bandari mbili hizi.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kufuatana na mimi kuona mazingira halisi ya usafiri pale katika bandari ya Mkokotoni kwa sababu TRA wako pale wanakusanya kodi?

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama amenisikiliza vizuri katika jibu langu la msingi hatua ambazo tunazichukua ya kwanza ilikuwa inajibu swali lake kikamilifu. Hatua zilizofuata tumeongeza mipango mingine tunayoifanya, kwamba *SUMATRA* hufanya ukaguzi kila mwaka, vilevile hufanya kaguzi za kushtukiza kuhakikisha kwamba vyombo hivi vinavyoelea majini vinakuwa na usalama wa abiria na mizigo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili niko tayari, tutapanga tukubaliane siku ya kwenda na tukaelee majini kati ya Bandari ya Tanga na Mkokotoni ili tukubaliane haya ambayo Serikali inayasema na Mheshimiwa Mbunge anadhani kwamba hatuyajibu kikamilifu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa Mbaraka Dau.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti,

ahsante. Nakubaliana na Waziri kwamba suala la kwanza ni ukaguzi, lakini kwa kweli suala la ujuzi na utaalim ndio muhimu sana katika uokozi.

Je, Serikali imejiandaa vipi katika suala hili la kutayarisha umma na wataalam wa kuweza kufanya uokozi kuliko kungojea kutibu badala ya kuzuia?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumeongelea umuhimu wa shughuli za *SUMATRA* na hapa tuliongelea masuala ya ukaguzi, lakini unafahamu kwamba *SUMATRA* wana kituo kikubwa Dar es Salaam ambacho kinashughulika na masuala ya uokozi katika bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki vilevile kina vituo vidogo Mwanza na wanawasiliana na vituo vingine vya sehemu mbalimbali katika Bahari ya Hindi ili kuhakikisha kwamba kama kunatokea tatizo lolote vyombo hivi ambavyo vinashirikiana hata na wenzetu wa *Marine Service* kuhakikisha kwamba usalama wa baharini unakamilika. Mheshimiwa Ally Saleh unafahamu kuna *tower* kubwa sana kwenye Bandari ya Dar es Salaam kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba ina-*coordinate* shughuli zote za uokozi na wataalam tunao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya usafiri wa baharini ya Bumbwini yanafanana sana na matatizo ya usafiri baina ya Bandari ya Kilindoni, Mafia na Bandari ya Nyamisati, Kibiti. Wananchi wa Mafia wamekuwa wakisafiri katika maboti ya mbao ambayo si salama na hayana bima.

Je, ni lini Serikali itainunulia Wilaya ya Mafia boti ya kisasa kuondokana na tatizo la usafiri baina ya Bandari ya Nyamisati na Kilindoni ili kuepusha maafa? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbaraka Dau anafahamu kwamba Serikali ina mikakati maalum ya kuhakikisha inatutua tatizo la usafiri Mafia. Tukianza kuhakikisha kwamba magati yanayotumika ni ya kisasa na yako salama. Kwa vyovyote vile magati haya yakishakaa salama tutavutia wawekezaji wa kuleta meli na kama ikitokea kwamba hakutakuwa na meli zitakazofika, pamoja na kuimarisha gati kwa maana ya gati iliyoko tayari pale Mafia, lakini vilevile hili linalopokea upande wa Bara, tukishakamilisha hizo kama hatutakuwa na wawekezaji binafsi watakaovutika kutoa huduma za usafiri nikuhakikishie Mheshimiwa Dau tutakaa pamoja tuangalie tufanyeje pamoja na Serikali tuone namna ya kutatua usafiri wa eneo hili la Mafia. (*Makofi*)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja ya msingi ambayo inaonekana ni usalama wa raia wakati wakivuka. Mbunge wa Mafia alisema kutoka Nyamisati na Kilindoni, maboti yaliyoko pale ni maboti ya mbao, Serikali ina mikakati ya mrefu ufumbuzi haupatikani.

Swali la msingi sasa, Serikali ina mkakati gani wa ziada sasa kuhakikisha maboti haya yanayochukua abiria yamepewa uwezekano wa kuwa makoti ya kuokolea maisha (*life jacket*) ili kunusu maisha ya abiria?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Mbarawa majibu kwa ufupi sana.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tukianza na lile swali la Mheshimiwa Dau, Serikali ina mpango wa kupeleka kivuko eneo lile, kwanza kazi inayofuata ni kufanya *feasibility study*, baada ya kufanya *feasibility study* na kujua bei ya hicho kivuko *then* tutapanga pesa kwa ajili kununua kivuko hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa Masoud ni kweli kwamba kuna tatizo hilo na tutahakikisha kwamba sasa hivi tunapeleka vyombo vyote kuhakikisha kwamba vinakuwa na *life jacket* ili ikitokea matatizo wananchi wale waweze kujisaidia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Massay wa mwisho.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa swali la msingi linahusiana na usalama wa wasafiri, na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri aliahidi kuja maeneo ya Mbulu na kwa kuwa ile barabara ya lami ya kilometa tano ya Hydrom na Dongobesh bado. Je, Mheshimiwa Waziri lini sasa atakuja Hydrom kuangalia barabara ile ambayo haina usalama kwa wasafiri? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Hujalisikia swali vizuri? Mheshimiwa Massay naomba urudie. Basi Mheshimiwa Waziri atalijibu amelisikia.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge na niko tayari wakati wowote kwenda kutembelea eneo hilo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Victor Kilasile, Mbunge wa Lupa aulize swali lake.

Na. 355

Sera ya Magari ya Serikali

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Je, ni nini Sera ya Magari ya Serikali?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magari ya Serikali, kama ilivyo kwa mali zingine za Serikali samani, ardhi na majengo, madini, misitu, uoto wa asili na kadhalika husimamiwa na sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha menejimenti ya mali za Serikali, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imeanza kuandaa Sera ya Menejimenti ya Mali za Serikali (*Government Asset Management Policy*). Sera hiyo ambayo inaandaliwa chini ya uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango itasimamia menejimenti ya mali zote za Serikali yakiwemo magari. Sera hiyo pamoja na mambo mengine itaelekeza utaratibu mzima wa ununuzi, utunzaji na ufutaji/uondoshaji wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inaendelea kukamilisha Sera hiyo, ununuzi, utumiaji na uondoshaji wa magari ya Serikali utaendelea kusimamiwa na Sheria ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma Sura ya 410 na kanuni zake, Sheria ya Fedha na kanuni zake pamoja na miongozo inayotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa magari yote ya Serikali hununuliwa kwa pamoja (*bulk procurement*) ili kuipunguzia Serikali gharama za ununuzi. Kwa mujibu wa sheria ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma, Sura 410, Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi wa Serikali (*GPSA*), ndiyo yenye dhamana ya ununuzi baada ya kupata kibali cha ununuzi wa magari hayo toka Ofisi ya

Waziri Mkuu kwa kuzingatia viwango (*specifications*) vinavyotolewa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma pamoja na kanuni zake, matengenezo na usimamizi wa matengenezo ya magari yote ya Serikali hufanywa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*). Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, miongozo inavyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma uondoshaji (*disposal*) wa magari ya Serikali katika matumizi ya umma hufanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikisha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Victor swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu, vilevile napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa azma yake ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Vilevile kwenye *issue* ya magari naipongeza Serikali kwa kuamua kununua kwa wingi (*bulk procurement*) ambayo inapunguza bei, na vilevile kununua kwa mtengenezaji badala ya kununua kwa mtu wa katakati ambayo nayo inapunguza bei, nawapongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza.

Sasa hivi Serikali pamoja na kwamba haina sera ya magari, magari mengi yanayotumika ya Serikali ni Toyota, bei ya *Toyota Land Cruiser VX* bila ushuru ni shilingi milioni 220. Bei ya *Toyota Land Cruiser Prado* ambazo kwa sifa zote zinafanana ni shilingi milioni 120 bila kodi. Kwa hiyo, Serikali ikiamua kununua magari 20 ya *VX* na ikaacha ikanunua *Prado* ita-save karibu shilingi bilioni mbili ambayo inaweza ikatatua matatizo ya maji katika Mji wa Chunya, Mji wa

Makongorosi hata Mkwajuni kwa Wilaya mpya ya Songwe. Je, Serikali inasemaje kuhusu kuachana na VX na kutumia Prado kwama inavyotumia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar? (Makofi)

Swali la pili, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Serikali inafuata Sheria ya Udhhibiti na Ununuzi wa Mali ya Umma Sura ya 410. Sheria hiyo inasisitiza ununuzi wa mali ya umma ni kwa *tender* na *disposal* ya mali ya umma ni kwa *tender*. Zamani ilikuwa magari ya Serikali yale yanayochakaa yanakusanywa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba uliza swali.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Magari yanakusanywa *MT Depot* na yanauzwa kwa *tender*. Siku hizi hawafanyi isipokuwa Idara ya Usalama wa Taifa ndio inauza kwa *tender*.

Serikali inasemaje kuhusu Viongozi wa Serikali ambao wanajiuza magari yaliyochakaa badala ya kuuza kwa *tender*? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema masuala ya ununuzi wa magari ni masuala yanayosimamiwa na sheria vilevile Wizara ya Fedha ndio inayosimamia *GPSA*. Kwa maana hiyo, nachukua maoni yake tutaenda tukayafanyie kazi kwa kushirikisha *GPSA* pamoja na Wizara ya Fedha pamoja na Idara Kuu ya Utumishi ili hatimaye tupate majibu sahihi na hatimae nitakueletea hayo majibu sahihi Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Waziri una majibu ya ziada? Mheshimiwa Waziri naomba utoe maelezo ya ziada.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuongezea kidogo hasa kuhusu magari baina ya *Toyota Prado* na *Landcruiser VX*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati unanunua kitu unaagalia mahitaji yako, kwanza unangalia bei, unaangalia *safety*, unaangalia *maintainance cost*, vitu vyote hivi unaviangalia baada ya hapo ndio unaweza kupima. Ukinunua gari baina ya Zanzibar na Bara ni mazingira tofauti, magari yanayotumika Zanzibar yanatumika kwa siku pengine kilometa 30, hapa mtu anasafiri takribani kilometa 200, 300 mpaka 500 mpaka 1,000 kwa siku, 1,200 naambiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ukinunua gari inabidi vitu vyote hivi uviangalie, sio uangalie *price* tu. Uangalie *comfort*, uangalie *safety*, uangalie *mainatainance cost* na vitu vingine vyote. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi sasa aulize swali lake.

Na. 356

Tatizo la Nyumba za Askari

MHE. STANSLAUS S. MABULA (K.n.y. MHE. AMINA N. MAKILAGI) aliuliza:-

Je, nini mipango ya Serikali ya kumaliza tatizo kubwa la nyumba za askari hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna tatizo kubwa sana la nyumba za Askari za kuishi. Kwa kufahamu hilo Serikali imekuwa ikitenga bajeti ya ujenzi wa makazi ya Askari kwa awamu kulingana na uwezo uliopo. Aidha pamoja na kutenga fedha hizo Wizara yangu itajielekeza zaidi kutumia rasilimali zilizopo na teknolojia rahisi ya ujenzi wa nyumba ili kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ubia baina ya Serikali na sekta binafsi Jeshi la Polisi limefanikiwa kujenga nyumba 353 Kunduchi na Mikocheni, Dar es Salaam kwa ajili ya askari wa kawaida na maafisa. Aidha, Jeshi la Magezea linaendelea na ujenzi wa nyumba 320 Ukonga, Dar es Salaam kwa fedha za Serikali na lipo katika mazungumzo ya ubia na Shirika la Nyumba la Taifa utakaowawezesha kujenga nyumba 100 Msalato, Dodoma. Kadhalika, Idara ya Uhamiaji inafanya makubaliano na Shirika la Nyumba la Taifa kwa ajili ya ununuzi wa nyumba 103 Dodoma, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la kuhamia Dodoma. Utaratibu huu utaendelezwa katika Mikoa mingine ili kupunguza changamoto hii kwa Askari wetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stanslaus Mabula swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwa kuwa Serikali inakiri kuwepo na tatizo kubwa la upungufu wa nyumba za makazi ya askari polisi na vyombo vingine ambavyo viko ndani ya Jeshi la Mambo ya Ndani. Serikali haioni sasa mipango na mikakati iliyonayo bado haiwezi kuwa ni kigezo cha kukamilisha tatizo hili kubwa tulilionalo nchini?

Swali langu la pili, pamoja na matatizo haya ziko nyumba ambazo zimeshaanza kujengwa takribani miaka mitano leo, zikiwemo nyumba za *Mabatini Barracks* katika Jimbo la Nyamagana na maeneo mengine kama Musoma na Mikoa mingine yenye matatizo kama haya.

Je, ni lini Serikali itahakikisha nyumba hizi ambazo zikikamilika kwa wakati kwanza tunaoko upotevu wa fedha nyingi, lakini inasaidia watu wetu wanaohangaika kutafuta makazi kukaa kwenye makazi yaliyo bora na kuwafanya wafanye kazi yao kwa uaminifu na uhakika zaidi?
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na mradi wa nyumba ambazo zipo katika Jimbo lake nikiri kwamba nyumba zile zimefika katika hatua za mwisho kukamilika. Mimi na yeye tuliwahi kufanya ziara kutembelea, tuliona kwamba kuna umuhimu wa nyumba zile kukamilika kwa haraka ili kuweza kutatua tatizo la makazi katika eneo la Nyamagana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Nyamagana tu, tuna nyumba maeneo mbalimbali nchini ambazo zipo katika hatua za kukamilika, ikiwemo Musoma Mjini, Kagera, Mtambaswala huku Mtwara, Ludewa na kadhalika. Kwa hiyo, kwa kutambua kwamba kuna haja ya kumaliza nyumba hizi ambazo zimefika katika hatua nzuri katika bajeti ya mwaka huu ya maendeleo ambayo tumetenga takribani zaidi ya shilingi bilioni 5.2 malengo ni kukamilisha miradi hii ambayo imefika katika hatua nzuri na za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatarajia katika kipindi cha mwaka huu wa fedha tutamaliza *project* ile ya Nyamagana (Mabatini) pamoja na nyingine ambazo nimezitaja. Kwa hiyo, ni miongoni mwa mikakati ya Serikali ya kutatua matatizo ya nyumba za askari nchini.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa vile watu wengi sasa wanaotaka swali la nyongeza, nashauri tu mngemuona Mheshimiwa Waziri kwa wakati wenu mkamuuliza kwa sababu hatuwezi kuwapa upendeleo itakuwa ni mgumu hapa. Tunaendelea na swali la

Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 357

Hitaji la Ofisi ya Wilaya ya Kipolisi Mbalizi

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y MHE. ORAN M. NJEZA) aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini wanaipongeza Serikali kwa kuanzisha Wilaya ya Kipolisi Mbalizi.

(a) Je, ni lini Ofisi ya Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi itajengwa zikiwemo nyumba za kuishi askari?

(b) Je, Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi ina magari mangapi na Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya vituo vya polisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua ukosefu wa Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya na ukosefu wa nyumba za kuishi askari Wilaya ya Kipolisi Mbalizi. Ni lengo la Serikali kukamilisha ujenzi wa vituo vya polisi kwenye wilaya 65 zilizosalia na ujenzi wa nyumba za makazi. Ujenzi huu utatekelezwa kwa awamu kutegemeana na upatikanaji wa fedha zitakazotengwa katika bajeti kila mwaka na kutumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi ina magari mawili, moja liko Mbalizi na lingine lipo kituo kidogo cha Inyara. Serikali itaendelea kuboresha

miundombinu ya Vituo vya Polisi katika Halmashauri ya Mbeya na kwingineko kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyoongezeka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Oran swali la nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama kwa niaba ya Mheshimiwa Oran ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mbeya kijiografia imekaa vibaya sana, vituo vingi zaidi hasa katika Kata ya Igoma Tarafa ya Tembela pamoja na kule Isangati hakuna vituo vya polisi kabisa na jiografia yake kama nilivyosema ni mbaya. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alikuwa ameahidi kabisa kwamba vituo hivi vijengwe, lakini mpaka leo hakuna. Nataka kujua majibu ya Serikali ni lini itajenga Vituo vya Polisi huko Igoma pamoja na Ilembo katika Tarafa ya Isangati?

Swali la pili, Wabunge wa Mkoa wa Mbeya wote kwa pamoja tunachanga kwa juhudi zetu na wananchi kujenga Kituo cha Polisi cha Mbalizi. Ninataka kujua ni nini mkakati wa Serikali katika kuongeza nguvu katika kituo hiki cha Polisi Mbalizi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hili na Wabunge wa Mkoa wa Mbeya ambao wameshirikiana katika kujenga kituo hiki. Binafsi nilikwenda pale kuzindua ujenzi huo na sisi vilevile tulichangia, lakini niwapongeze pia, wananchi wa Mbeya kwa kuweza kujitolea kukijenga kituo hiki katika hatua ambayo sehemu iliyofikia ni karibu asilimia 50 ya ujenzi imekamilika na huu ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, changamoto ambayo ameizungumza katika maeneo mengine ya Isangati, nitoe changamoto kwamba wakiendelea na jitihada kama hizi itasaidia kuharakisha ukamilishaji wa ujenzi wa vituo katika maeneo mengine kwa haraka ili kusaidia kukamilisha dhamira njema ya Serikali ya kukamilisha ujenzi wa vituo 65 nchi nzima vyenye mapungufu katika maeneo mbalimbali nchini.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 358

Utaratibu wa Kutoa Ruzuku ya Pembejeo kwa Njia ya Vocha

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo kwa njia ya vocha kwa lengo la kuwasaidia wakulima, lakini utaratibu ukiwanufaisha Mawakala wa Mbolea kuliko wakulima ambao ndio walengwa.

Je, Serikali inachukua hatua gani ya kuweza kubadilisha utaratibu huo na kuja na utaratibu mwingine utakaoweza kuwasaidia wakulima?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI,VIJANA NA AJIRA (K.n.y WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine, Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho ya utaratibu wa vocha ulitumika msimu wa mwaka 2013/2014

na mwaka 2014/2015, utaratibu uliotumika ulikuwa wa vikundi na msimu wa 2015/2016 utaratibu wa vocha ulitumika tena kwa kuwa wakulima wengi hawakuwa kwenye vikundi na hivyo kutonufaika na ruzuku. Aidha, Serikali msimu wa mwaka 2016/2017 imetumia Kampuni ya Mbolea ya *TFC* kusambaza ruzuku ya pembejeo moja kwa moja kwa wakulima kupitia mawakala waliowachagua wao wenyewe na waaminifu na sio kutumia vocha tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeunda Kanuni ya Uingizaji mbolea kwa wingi (*Bulk Fertilizer Procurement Regulation 2017*) kwa kuanza na mbolea za urea na *DAP*. Lengo ni kuwa uagizaji huu utasababisha mbolea kushuka bei na hivyo Serikali kutokulazimika kutoa ruzuku ya mbolea hizo. Utaratibu huu utaendelea kutumika kwa aina nyingine endapo zitakidhi kanuni hiyo, hususan uwingi wa mahitaji yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 19/05/2017 awamu ya kwanza uchambuzi wa wazabuni ilifanyika, kati ya kampuni 20 zilizoomba kampuni 17 zimepitia awamu ya kwanza, kati yake kampuni kumi ni za ndani na Saba ni za nje ya nchi. Hii inaonesha muitikio mkubwa wa waagizaji wa utaratibu huu na hivyo matarajio ni bei kushuka na kila mkulima kujinunulia. Utaratibu mwingine ni kuwa Serikali inahimiza ujenzi wa viwanda vya mbolea hapa nchini ili kuondokana na uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Josephine swali la nyongeza halafu Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza naipongeza Serikali kwa kubadilisha utaratibu wa awali kwa sababu utaratibu wa awali wakulima waikuwa hawanufaiki. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa msimu wa mvua

katika maeneo mbalimbali hapa nchini unatofautiana, kwa mfano, katika Mkoa wa Kigoma mvua za kupandia ni za mwezi wa Oktoba. Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima mapema zaidi kuliko ilivyo sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wapo mawakala waliofanya kazi kubwa ya kusambaza mbolea kwa wakulima. Na kati ya mawakala hao wapo waliofanya kazi kwa uadilifu mkubwa na uaminifu, lakini wapo ambao hawakuwa waaminifu na Serikali ilituma watu kwenda kuhakiki madeni kwa mawakala hao nchi nzima.

Je, ni lini Serikali itawalipa mawakala waliofanya kazi kwa uadilifu, ili waweze kulipa madeni waliyokopa katika benki mbalimbali, wakiwemo mawakala wanawake ambao wanateseka sana kudai pesa zao? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza la kuhusu utofauti wa misimu ya mvua na mbolea kuwafikia wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Wizara ya Kilimo inatambua kwamba pembejeo ya mbolea ni kati ya virutubisho muhimu sana, ili kumfanya mkulima wa Kitanzania aweze kulima kilimo cha tija. Sasa katika mpango wa Wizara ni kuhakikisha kwamba katika mfumo huu mpya ambao tunakwenda nao wa *bulk procurement* mbolea hizi ziweze kuwafikia wakulima kwa wakati, ili waweze kutumia kwa ajili ya kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu ya *Maputo Declaration* ya mwaka 2003 ambayo katika Ukanda wa Nchi za Kusini mwa Afrika imesema kwamba Tanzania ni kati ya nchi ambazo zinatumia kiwango kidogo cha virutubisho kwa hekta moja ambayo kwa mujibu wa *Declaration* hii inapaswa kila hekta moja vitumike virutubisho kilo 50 na sisi tupo katika kilo 19. Kwa hiyo, kwa kuona umuhimu huo

Serikali sasa itahakikisha kwamba, mbolea hii inawafikia wakulima kwa wakati, ili waweze kulima kilimo cha tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili amezungumza kuhusu uhakiki wa malipo ya mawakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Waziri wa Kilimo wakati wa bajeti yake ni kweli, wako mawakala ambao walifanya kazi hii kwa uaminifu, lakini ambao bado hawajalipwa malipo yao. Tayari Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kufanya uhakiki kwa Mikoa yote 26, isipokuwa Dar es Salaam peke yake ili ndani ya mwezi mmoja mawakala hawa ambao walisambaza pembejeo waweze kulipwa pesa zao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Dkt. Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa tunaona dhahiri kwamba kilimo kinazidi kurudi nyuma badala ya kusonga mbele, na kwa kuwa tumekuwa sasa wakulima hasa wale wa vijijini wanategemea mbegu za kununua na sio mbegu za asili na mbegu hizi zinaenda sambamba na upatikanaji wa mbolea. Siku hizi kuna mbolea ya kulimia, kuvunia na kadhalika, wakati kilimo cha zamani cha asili tulikuwa tunatumia mfano, mbolea za samadi na mbegu zenye ubora.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurudi nyuma na kujitathmini kwamba tunakoenda siko, tuangalie zile *system* za zamani za kilimo ziboreshwe zaidi ili wakulima wapate manufaa ya mazao yao? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI,VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ushauri ambao ameutoa na kama Serikali tumeuchukua.

Katika mpango wa Serikali katika huu mfumo mpya

unaokuja wa *bulk procurement* Serikali itaagiza kwa wingi mbolea ya kupandia ambayo ni *DIP* na mbolea ya kukuzia ambayo ni *urea*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea nyinginezo kwa maana ya *NPK, MOP, SA* na *Bio fertilizers* na *folia* zile za maji, hizi zitakuja katika utaratibu wa kawaida. Vilevile ndani ya Wizara ya Kilimo yupo Wakala wa Mbegu ambaye kazi yake ni udhibiti wa mbegu bora ambaye ni *ASA* na yeye tutamtumia ili wakulima wetu wafanye kilimo chenye tija.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tunamalizia. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini asasa aulize swali lake.

Na. 359

Umuhimu wa Kupima Ardhi – Mji wa Tarime

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Ardhi ikipimwa huwa na thamani na hivyo kuwafanya wamiliki kupata mikopo katika taasisi za kifedha na kuwekeza katika uchumi. Katika Jimbo la Tarime Mjini ni Kata mbili tu za Bomani na Sabasaba ndizo ambazo ardhi yake imepimwa kwa asilimia 75 kati ya kata nane zilizopo, hii inatokana na upungufu mkubwa wa wataalam wa kupima ardhi.

Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam wa kutosha ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tarime kuweza kupima ardhi kwa kata sita zilizosalia ili wananchi wa Tarime Mjini waweze kunufaika na ardhi yao?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu

swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, swali lake Na. 359 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kupanga na kupima ardhi nchini kwa manufaa ya wananchi wake. Halmashauri ya Mji wa Tarime ina wataalam wa ardhi wanne tu ambao ni Afisa Mipango Miji, Afisa Ardhi, Mchora ambaye ni Mrasimu Ramani na Mthamini Mali. Idadi hii ni ndogo ukilinganisha na kasi ya ukuaji wa Mji wa Tarime kwa sasa. Tatizo hili si kwa Mji wa Tarime pekee bali ni tatizo linalozikabili karibu Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kutekeleza azma ya kupanga na kupima kila kipande cha ardhi kwa nchi nzima, ikiwemo kusajili makampuni binafsi ya kupanga ardhi, yenye weledi wa kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Hadi sasa tuna jumla ya makampuni 36 ya kupanga miji na makampuni 65 ya kupima ardhi yamesajiliwa ili kuongeza kasi ya upangaji na upimaji wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaandaa utaratibu wa kuwatumia wataalam wa sekta ya ardhi kutoka katika maeneo yenye watumishi wa kutosha kufanya kazi katika maeneo yenye uhaba mkubwa wa watumishi na hivyo kuharakisha kasi ya upangaji na kupima ardhi nchini. Halmashauri ya Mji wa Tarime ni mojawapo ya maeneo yanayotarajiwa kunufaika na utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia inaendelea kuzihimiza Halmashauri zote nchini kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao kwa ajili ya kuajiri wataalam wa sekta ya ardhi wanaokidhi mahitaji na hivyo kuongeza kasi ya kupanga na kupima ardhi katika maeneo yao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti,

nakushukuru. Nashukuru kwamba, Wizara inatambua kwamba Mji wa Tarime unatakiwa kupimwa, lakini pia inatambua kwamba una upungufu wa watumishi. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo mengi ya Mji wa Tarime yalikwishaandaliwa ramani ya Mipango Miji, lakini mpaka sasa hivi hayajapimwa, na kwa kuwa wananchi wanaendelea kujenga kiholela na kuharibu ramani ambayo tulikwishaandaa hapo awali, ni kwa nini sasa Serikali msiweze kuunda kikosi kazi kwa ajili tu ya kuja kupima maeneo yote ambayo yameshaandaliwa ramani ya mipango miji ili sasa tusiharibu hii ramani ambayo imeshaandaliwa?

Swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Tarime haina vifaa vya kuweza kupima ardhi na tumekuwa tukikodi kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, na kwa kuwa, Halmashauri ya Mji wa Tarime hatuna fedha za kuweza kununua vifaa hivi ambavyo vinauzwa bei ghali sana, ni kwa nini sasa Serikali isiweze kufadhili ununuzi wa vifaa hivi ili kuweza kupima maeneo mengi zaidi na kuweza kuharakisha umilikishaji wa ardhi kwa wananchi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anasema maeneo mengi ya Tarime yalikuwa yamepimwa, yana michoro tayari, lakini upimaji wake pengine haujakamilika na yameanza kuvamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali hilo naomba nijibu kwamba kwanza niwaombe Halmashauri yenyewe husika kwa sababu ndio kwanza inazidi kukua sasa hivi, kama maeneo yale hayajakamilika katika upimaji niombe Halmashauri iwe makini katika kulinda yale maeneo yasivamiwe, kwa sababu katika maeneo yote yenye michoro wananchi wanapovamia, hapatakuwa na upimaji mpya. Maana yake wakikutwa wamevamia kiwanja kimoja watu wawili/watatu, maana yake pale lazima mmoja itabidi

apishe apewe kile kiwanja na mwingine atafutiwe eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanya lile eneo lisiingiliwe na watu wengi zaidi niwaombe sana Halmashauri kwanza wakamilishe ile taratibu kwa sababu ni jukumu pia la Halmashauri, lakini watasaidiwa pia na Ofisi yetu ya Kanda ambayo sasa hivi wamesogezewa, itakuwa iko Simiyu. Kwa hiyo, tukishafanya hivyo tutakuwa tumelinda yale maeneo. Urasimishaji unaofanyika hauwezi kufanyika katika yale maeneo ambayo tayari yalikuwa yamepimwa, unafanyika katika maeneo ambayo yapo katika ule utaratibu upo.

Kwa hiyo, suala la kuwa na vikosi kazi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kazi hii inafanyika haraka ni jukumu pia la Kanda husika kwa sababu, tunaweza tukatumia Wataalam walioko katika Halmashauri jirani wakiratibiwa na Ofisi ya Kanda, suala hilo linaweza likafanyika na inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la vifaa; suala hili nilishalijibu pia katika majibu ya nyuma katika Bunge hili. Niombe sana Wizara haiwezi kununua vifaa vya upimaji katika Halmashauri zote, ni jukumu la kila Halmashauri kuweka bajeti zake, Wizara imejipanga katika Kanda zake na vifaa vile katika Kanda vinaweza kutumika katika Halmashauri yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi vifaa vile vina bei kubwa sana, lakini ninaomba na nimekuwa nikielekeza wale wenzetu walioko kwenye Kanda, kila mmoja ana Halmashauri zake ni kiasi cha kupanga utaratibu mzuri, mkiwa na vikosi kazi ambavyo vinaweza vikasaidia katika kwenda Halmashauri moja baada ya nyingine itaturahisishia katika kupunguza kero ya upimaji.

Kwa hiyo, naomba pamoja na *private sector* ambao wanatumika, bado Ofisi zetu za Kanda kwa kutumia watumishi katika Halmashauri kwenye Mkoa husika tunaweza tukapunguza tatizo hilo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na muda wetu kwa maswali umeishia hapo.

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo, naanza na matangazo ya wageni ambao wapo Bungeni leo hii. Tunao wanafunzi 77 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Mlimwa, Mkoani Dodoma, karibuni. Pia tunao wanafunzi 41 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari Mtobubu iliyoko Wilayani Kondo, Mkoani Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 100 na walimu Watano kutoka Chuo cha Utalii Nchini cha Mkoani Dodoma, karibuni nanyi pia. Tuna wanafunzi 56 kutoka Chuo cha Mipango, Mkoani Dodoma, karibuni sana wageni wetu wote ambao mmetutembelea kwa siku hii ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapa pia nina tangazo moja kutoka kwenye Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore inawatangazia wakatoliki wote kuwa lbada ya siku ya leo terehe 7 Juni, 2017 itakuwa mara baada ya Bunge kuahirishwa na mnaombwa tafadhali mfike kwa wakati.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni la semina ya Wabunge wote wa CCM, semina hii iliyokuwa imepangwa kufanyika mara baada ya Bunge kuahirishwa sasa itafanyika saa saba mchana pale *White House*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zetu za leo zimeishia hapa, naomba niahirishe Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 4.26 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 8 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)